**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**
**Tovuti: www.hlpc.go.tz**
**Simu: 0750059900 Barua Pepe:hlpc@afya**

# TAARIFA KWA UMMA

## KUFUNGUA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI NOVEMBA 2025

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inawataarifu wahitimu wote wa Shahada ya Maabara ya Afya ya Binadamu ambao hawakuchagua vituo vya utarajali kuwa utaratibu wa kufanya maombi ya usajili wa awali na kuchagua vituo ni kama ifuatavyo,

- Hakikisha unafanya maombi ya usajili wa awali (Provision registration) kuanzia leo tarehe 10.11.2025 hadi 23.11.2025
- Dirisha la kuchagua kituo cha utarajali litafunguliwa tarehe 24.11.2025 saa 4:00 asubuhi na kufungwa tarehe 25.11.2025 saa 4:00 Asubuhi
- Siku ya kuchukua barua na mahitaji mengine kwa ajili ya kuripoti kituoni cha mafunzo itakuwa tarehe 28.11.2025 saa 2:00 asubuhi. Waliochagua vituo vya utarajali watafika ofisi ya Msajili iliyopo Wizara ya Afya, Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.

Aidha, Maombi yatafanyika kupitia mfumo wa ***hprs.moh.go.tz.*** Mhitimu hawezi kuchagua kituo cha utarajali kama hajafanya maombi ya usajili wa awali na maombi yake yawe yamefanyiwa kazi

**Mambo muhimu ya kuzingatia;**

1. Wakati wa maombi ya awali lazima mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa, cheti cha sekondari, barua ya utambulisho kutoka chuoni (alisoma chuo cha hapa nchini) au cheti cha uthibitisho kutoka TCU, cheti cha matokeo na cha chuo alichosoma kwa waliosoma vyuo vya nje ya nchi,

2. Waombaji wote wanasistizwa kufanya maombi kwa wakati na ikitokea mwombaji atahitaji kubadili kituo cha utarajali itampasa kutumia mfumo wa ***hprs.mo.go.tz*** kupitia akaunti yake. Pia kituo kikiwa hakina nafasi huwezi kuhamia. Aidha zoezi hili la kubadili kituo linatakiwa lifanyike kabla ya dirisha la maombi kufungwa baada ya hapo **HAKUTAKUWEPO NA UWEZEKANO** wa kubadili kituo cha utarajali tena.

Ofisi ya Msajili inawatakia waombaji wote utekelezaji mwema

Imetolewa na

Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
10.11.2025

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
10 NOV 2025
P.O. Box 743
DODOMA